

1. MAMILIONEA HUFIKIRIA KUPANGA MALENGO

“Janga la maisha haliko katika kupanga malengo na kutoyafikia. Janga lipo katika kutokuwa na malengo ya kuyafikia.” Benjamin Mays

Mamilionea wanajua kupanga malengo na siyo kufanya hili halafu lile wakati huo huo. Daima huwekeza akili na nguvu zao katika jambo la muhimu ambalo wakifanikisha litaleta maana maishani mwao. Huwa hawapangi malengo ya jumla bali humaanisha na kuzungumza kiwango au kiasi kamili. Kwa mfano husema nitakuwa ninaamka saa kumi na moja kamili asubuhi badala ya kusema nitakuwa ninaamka asubuhi na mapema. Umuhimu wa kupanga malengo ni kufanya utekelezaji kuwa rahisi kwa kuchukua vitendo vinavyotakiwa ili kuleta mafanikio. Ujue kuwa kuishi bila kuwa na malengo ni janga kubwa kwa maisha yako.

Lazima tuige mfano wa serikali, serikali husema inataka kujenga barabara. Inafanya upembuzi yakinifu, inatayarisha bajeti, inatafuta mkandarasi na kumweleza inataka ijengewe barabara ya kiwango cha aina fulani. Na kazi ikianza mpaka inamalizika, na maisha yetu yanatakiwa kuwa namna hiyo. Ndipo tutakapo ona mabadiliko makubwa katika maisha yetu. Les Brown alisema, ***“Kama ukipanga malengo na kuyatekeleza kwa kudhamilia kote, unaweza kuyatawala, zawadi zako zitakupeleka mahali ambapo patakushangaza.”***

Hivyo kuanzia saa hii unapomaliza kusoma aya hii. Amua kuanza kupanga malengo na malengo yenyewe yawe makubwa na fuatilia utekelezaji wake. Sema tarehe 30 mwezi wa kumi na mbili mwaka 2024 nitakuwa nimenunua kiwanja chenye thamani ya shilingi milioni mbili laki tano.

Hivyo kila mwaka nitaweka shilingi laki tano na ina maana kila mwezi nitaweka shilingi arobaini na mbili elfu tu. Huu ni mfano wa kupanga malengo. Malengo yanakupa ujasiri wa kuyaacha yasiyo na umuhimu wakati huu. Kwa lengo hili utaacha kutumia fedha hovyoya kwa vile umepanga lengo la kujenga nyumba.

Malengo huongeza hamasa na hamu ya kufanya, pia hufanya mtu ajiamini zaidi. Humpa mtu mwelekeo na mwisho. Yanakupa kuchagua yaliyo muhimu zaidi na hata maamuzi yako huwa wazi kwa vile unajua unakokwenda, unachofanya na matokeo yake. Scott Reed anasema, *“Hii hatua moja ya kuchagua lengo na kuling’ang’ania hubadilisha kila kitu.”* Hivyo elekeza nguvu, akili na juhudi kwenye lengo ambalo ukilitekeleza litakufungulia milango mingine. Hii ni miongoni mwa siri za kuwa milionea, kupanga malengo na kuyatekeleza.

Matendo. Kuanzia leo jenga tabia ya kupanga malengo katika maisha. Panga lengo moja leo na sema lini litakamilika, anza utekelezaji na ukilimaliza panga lingine.